| | |
|---|---|
| **JINA: …………………………………………..** | **ADM NO …………………………….** |
| **SHULE: ………………………………………** | |
| **TAREHE: …………………………………………..** | |
| **MUDA: MASAA 2 NA NUSU** | |

# kiswahili karatasi ya 3

## KIDATO CHA TATU MUHULA WA TATU

**ATIKA SCHOOL**

**ALL SEASONS**

**MAAGIZO**

1) Jibu maswali MATATU pekee
2) Swali la KWANZA ni la LAZIMA
3) Maswali mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki
4) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
5) Kila swali lina alama ishirini

## SEHEMU A: USHAIRI

**Jibu swali  la lazima**

**1**. ***Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali.***

Mungu naomba subira, subira nayo imani
Imani iliyo bora, bora hapa duniani
Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani
Hiani pamwe ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhulu
Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri wangu muwili
Muwili hata kiclari, kidari kuwa thakili
Thakili kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele
Muwele wa hitilafu, hitilafu ya nduwele
Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele
Milele kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vitomele vikwato
Vikwato pia maole, maole kufanya mito
Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto
Kitoto kilo vipele, vipele vyenye fiakuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka
Kutamka wazi vino, vino subira kutaka
Kutaka imani mno, mno n’sipate wahaka
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.

Mashaka haya ya leo, leo yawe yamepita
Yaniepita na vilio, vilia vipishe nyota
Nyota njema ing'arao, ing'arao kunikita
Kunikita salamani, salamani nikadata.

**Maswali**

a) Kwa nini nafsi neni inaomba subira na amani? (al.2)

b) Shairi hili ni la aina gani kwa kuzingatia (al.4)

(i) Mpangilio wa maneno

(ii) Mpangilio wa vina.

c) Kwa kutolea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (al.4)

d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (al. 4)

e) Kwa kutolea mifano, eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa kutekeleza arudhi. (al.6)

## 2.SEHEMU B: FASIHI SIMULIZI.

***Jibu swali la 2 au 3***

**2a**

i. Eleza maana ya ngomezi katika fasihi simulizi. (al.2)

ii .Eleza sifa nne za ngomezi (al.4)

iii.Taja aina nne za mazingira ambapo ngomezi ilitumika katika fasihi simulizi. (al.4)

**b** i.Eleza maana ya miviga.(al.2)

ii.Fafanua umuhimu wa mivigha kwa wanajamii.(al.8)

**3a**Tofautisha :

i.Lakabu

ii.Ulumbi

iii.Misimu (al.6)

**3b**

Mwanangu Ribe ni kuvuka mto

Kwenye shangwe na amani

John ulifikiri ni ndoto

Na hivi sasa wayaona kwa macho

Sera huyu ni mumeyo

Umtunze kwa mema na mabaya

John huyu ni mkeo

Umtunze kwa mema na mabaya

Pindi mjaliwapo

Mje mkitutizama

- Huu ni wimbo wa aina gani? Toa sababu. (al.2)

- Aina hii ya wimbo huwa na umuhimu gani katika jamii yako? (al.5)

- Andika hoja saba kuonyesha tofauti kati ya methali na vitendawili. (al.7)

**4.SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

***Pauline kea: Kigogo***

"Atawasili kabla ya sherehe hizo."

a.Eleza muktadha wa maneno haya. (al.4)

b.Sherehe zinazorejelewa hapa ni gani? (al.2)

c.Kuwasili kwake kutakuwa na umuhimu gani.(al.4)

d.Anayewasili atakuwa anatoka wapi? (al. 2)

e.Fafanua maudhui yoyote mawili yanayojitokeza katika dondoo hili. (al.4)

f.Jadili hatima ya huyu anayengojewa kuwasili. (al.4)

5.Fafanua njia anazotumia majoka kuendeleza uongozi wake dhalimu (ala 20)

**Au**

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**Kenna Wasike: Mapenzi ya kifaurongo**

**Jibu swali la 6 au 7**

**6**

"Mwili mzima unaanza kutetemeka kama ndama aliyenyeshewa na vua kubwa,"

a.Yaweke maneno haya katika muktadha wake.(al. 4)

b.Eleza mbinu mbili zilizotumiwa katika muktadha huu.(al. 4)

c.Eleza sifa zozote saba za anayerejelewa na usemi huu. (al.7)

d.Eleza umuhimu wa anayerejelewa na muktadha huu.(al.5)

**Au**

**7**.Kwa kurejelea hadithi ya mapenzi ya kifaurongo , eleza jinsi maudhui ya nafasi ya mwanamke yalivyoshughulikiwa.(al.20)

## SEHEMU E: RIWAYA

**(Chozi la Heri)**

8.“Mbona huna bashasha za kijana wa umri wako.”

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (ala 4)

b) Ni yapi yalifuata baada ya maneno haya. (ala 12)

c) Eleza sifa nne za msemewa (ala 4)

9.Jadili maudhui ya Mauti katika riwaya ya Chozi La Heri. (Ala 20)